**MAELEZO.** Kutumika kwa maneno **“Mara saba”** kwa mara nyinngi hakumaanishi mara saba. **“Saba”** katika maandiko inamaanisha ukamilifu wa adhabu yao; basi hii inatumika kuonyesha mkazo, Ukamilifu wa kuadhibiwa kwao. Mara saba (siku moja kwa mwaka - Ezekieli 4:5, 6) au 2,520 pamoja na uhamisho wa Babeli chini ya Nebkadineza mwaka wa 486 B.C., na iliishia na uokoaji wa Waturuki chini ya Jenerali Allenby katika vita vya kwanza vya dunia, mwaka wa 1914.

5. Kwa kipindi cha miaka mingi ni nini ilisemwa kuhusu ardhi yao? Walawi 26:31-35.
6. Adhabu hii kali itawasababisha wafanye nini? Mstari 28, 29.
7. Je, ni maonyesho gani mengine yanaonyesha ukali wa adhabu yao? Yeremia 31:27, 28.
8. Katika hii miaka ya uhamisho, walikuwa aje mbele ya Elohim? Mstari 35-37.
9. Je, ni nini ilisemwa kuhusu utambulisho wao miongoni mwa mataifa katika kipindi hiki? Isaya 61:9
10. Je, maana hasa ya taabu hii ni nini? Hosea 5:15.
11. Kwa nini Elohim hakuwaharibu kabisa katika hii miaka? Walawi 26:44, 45.
12. Je, ni unabii gani wa Daudi unatimizwa sasa? Zaburi 102:15, 16.

******************************



**Somo la Julai 25, 2020 (Av 4, 5780)**

## KUTAMBUA ISHARA ZA NYAKATI ZETU

**Somo kuu: Mathayo sura ya 24.**
**Fungu la kukariri: Mathayo. 24:33**

1. Ni nani alikuja kwake Masihi akitafuta ishara? Mathayo 16:1
2. Alijibu nini? Mstari 2, 3.

   **MAELEZO**: - Mwokozi aliwaita mafarisayo na masadukayo wanafiki kwa sababu walijua hali ya anga, lakini hawakujua kuhusu ishara za nyakati. Hawakujua kitu kuhusu ukamilifu wa unabii wa biblia kuhusu matukio ya nyakati.

3. Ni swali gani muhimu wanafunzi walimuliza Mwokozi muda mchache kabla ya kusulubishwa kwake? Mathayo 24:3.
4. Jibu lake lilikuwa ni nini? Mistari 4-9.
5. Aliwaambia nini juu ya hali ya kiroho katika ulimwengu? Mstari 12.
6. Aliwaambia ni kazi gani itafanyika kabla ya kurudi kwake? Mstari 14.
7. Vipi kuhusu manabii wa uongo (wahubiri wa uongo), siku za mwisho, hatari ya kudanganywa siku za mwisho, – Mstari 24.





***"Utakieni Yerusalemu amani; Na wafanikiwe wakupendao" Zaburi 122:6***



# Masomo Ya Bibilia

***kwa***

**KANISA LA ELOHIM (COG)**
**Siku Ya Saba (7th day)**

Robo Ya Tatu
2020

Ya
Julai, Agosti, Septemba.
**(Tamuz, Av, Elul, Tishrei)**

Watenda kazi wanahitajika,
Mavuno ni mengi, lakini watenda kazi ni wachache...

**Tuma maombi yote kwa S.L.P 568, Jerusalem — Israel**

8. Je atarudi kwa siri au kuja kwake kutafahamika na watu wote? Mstari 25 hadi 27; 1 Wathesalonike. 4:16.
9. Ni kwa muda upi Mwokozi anafananisha kuja kwake na nyakati za maovu? Mathayo. 24:37-39; Mwanzo6:5, 6.
10. Ni nini kuhusu mgawanyiko utakaotokea atakapokuja? Mathayo: 24:40, 41.
11. Ni nani waaminifu na watumishi wenye hekima katika wakati huo? Mistari 43-47.
12. Je! Ni ni kuhusu watumishi wengine ambao hawajui ishara za nyakati, na wanafanya sikukuu na wale wanaokunywa mvinyo wa babeli? Mistari 48-50.
13. Nini kitatokea kwa kundi hili la watumishi? Mstari 51.
14. Je, mabaki ya kweli katika giza yanahusiana na muda wa kuja kwake? 1 Wathesalonike. 5:3, 4.

*******************************

**Somo la Agosti 1, 2020 (Av 11, 5780)**

# HALI YA KIROHO KATIKA SIKU ZA MWISHO

**Somo: Mathayo 24:36-51.**
**Fungu la kukariri: Luka 17:26.**

1. Je, Yahshua alisema nini kuhusu hali ya siku za mwisho? Luka 17:26-326.



**MAELEZO:** Kama mji wa Yerusalemu ni sehemu iliyochaguliwa na Baba kwa ajili ya manabii wake kuishi, kwa Mwana wake kufa, na sehemu ambayo atarudi kutoka mbinguni, ni hivyo, na imekuwa hivyo, kujulikana kama nchi takatifu na mji mtakatifu. Kwa sasa ni mtakatifu zaidi kuliko kipindi cha Gabrieli na Mathayo walipouita mji mtakatifu.

*******************************

**Somo la Septemba 5, 2020 (Elul 16, 5780)**

# ADHABU YA ISRAELI NA KUREJESHWA KWAO

**Somo kuu: Walawi 26:1-31.**
**Fungu la kukariri: Luka 21:24.**

1. Je, ni baraka gani na ulinzi gani Israel waliahidiwa ikiwa watamtii Elohim? Walawi 26:3-12.
2. Ikiwa watashindwa kumtii, adhabu yao ingekuwa gani? Mistari 14-17.
3. Ni kwa muda gani wataadhibiwa? Mstari 18.
4. Je, ni maonyesho gani yanaonyesha ukali wa hukumu ya Elohim dhidi yao? Mithali 19, 21, 24, 28.



**Somo la Julai 4, 2020 (Tamuz 12, 5780)**

# UNABII, MWANGA KATIKA ULIMWENGU WA GIZA

**Somo kuu: 2 Petro 1.**
**Fungu la kukariri: 2 Petro 1:21.**

1. Maandiko matakatifu yalitolewaje? 2 Timotheo 3:16.
2. Yalitolewa kwa malengo gani? 2 Timotheo 3:17.
3. Yaliyotabiriwa kwenye biblia yanatuongoza katika maisha ya kila siku na wakati uliopo? Yatafanyaje? Kumbukumbu la Torati 29:29.

**MAELEZO:** Asilimia kubwa ya maneno ya biblia ni unabii. Yaliyoyatabiriwa kitambo yanahusu leo kabla tu ya "kuja kwake Masihi mara ya pili". Hata hivyo matumaini yetu na imani yetu kwa Baba yetu wa mbinguni na Yahshua, mwanawe, ni unabii - ufufuko wa wafu; uzima wa milele; hata kutangazwa na malaika wakati wa kuzaliwa kwake, " amani duniani na nia njema kwa watu wote" hata hivo hakuna cha kudhuru wala kuharibu. Hapatakuwa na mateso, maombolezo au huzuni – hakutakuwa na kifo wala maumivu. Haya ndio matamanio na matumaini, yote ni unabii.



9. Paulo alifundisha kuwa kutakuwa na ufufuo wa wafu? Ni katika hali gani watafufuka? 1 Wakor. 15:42-44.
10. Je, ni nini Martha alisema kwa Yahshua baada ya kuwa amezungumza naye juu ya kifo cha Lazaro? Yohana 11:21-24.

**MAELEZO**. Sio mbali sana kutoka Bahari ya Galilaya, wachimbaji waligundua sakafu ya Kanisa, na baadhi ya samani ya mawe. Sakafu hiyo imeandikwa kwamba Kanisa hilo lilijengwa kwa heshima ya muujiza wa Yahshua kuwalisha watu 5,000 kwa mikate 5 na samaki 2 (Mathayo 14:15-20), na vilikusanywa vikapu 12 vya mabaki. Ufufuko wa wafu ni jambo rahisi sana kwa Baba, kama vile muujiza wa kulisha watu 5,000 kwa Bwana Yahshua. Masihi.

*******************************

3. Je, Yerusalemu ulikuwa ni mji wa namna gani, na uliongelewaje? Nehemia 11: 1, 18.
4. Je, nabii Isaya aliutaja kama mji mtakatifu? Isa. 52: 1
5. Baada ya Daniei kupelekwa Babuloni, na Yerusalemu kuangamizwa kwa sababu ya uovu wa watu, jinsi gani malaika Gabrieli aliuzungumzia Yerusalemu? Je, aliuita mji mtakatifu wakati huo? Danieli 9:21-24.
6. Bila kujali uovu wa watu wa Yerusalemu wakati wa Mwokozi wetu, uliongelewaje na Mathayo? Mathayo. 4:5.
7. Ni kwa ukuu gani wa maneno Yahshua aliutumia kuonyesha ukaidi wa watu? Mathayo: 23:37.
8. Ingawa watu hawa walimsulubisha, jinsi gani roho mtakatifu aliongea kuhusu Yerusalemu wakati matukio hayo yalirekodiwa? Mathayo. 27:52, 53.
9. Kama matokeo, ni nini ingekuwa adhabu yao kubwa? Mathayo 24:1-2; Luka 21:20-24.

**MAELEZO:** Uharibifu huu mbaya Kwa Yerusaremu ulitimizwa 70 A.D., wakati Tito, Jenerali, alipokuja dhidi yao.

10. Wakati Mataifa watakopoikanyanga, uliongelewa kama mji mtakatifu? Ufunuo 11:2.
11. Baada ya muda wa watu wa Mataifa kuisha, Je, ahadi kwa Yuda na Yerusalemu itakuwa gani? Zakaria 2:12, 13.



2. Je, hali ya ulimwengu katika wakati wa Nuhu ilikuwa gani katika mambo ya kiroho? Mwa. 6:5-8.
3. Je, siku za wakati wa Lutu zilikuaje? Mwa 19:13; 2 Petr. 2:6-8.
4. Paulo alielezea vipi hali ya kiroho katika siku za mwisho? 2 Tim 3:1-5.

**MAELEZO**. - Hii inaeleza kwa uwazi kabisa kuhusu hali katika wakati wa sasa, kuwa na tamaa na rushwa. Watu wanapenda anasa za ulimwengu, na wasiojali wengine, lakini wenye kujipenda wenyewe. Ni wana wa Bwana wachache tu, ndio wanaojitolea kwa wengine, hili wasikie maneno ya uzima wa milele na kuokolewa.

5. Jinsi gani Paulo alisema kuhusu watu kuzingatia ukweli na mafundisho ya kweli katika nyakati hizi? 2 Tim 4:3, 4.
6. Je, hali ya kiroho ni gani kwa kipindi cha mwisho katika vipindi saba vya kanisa, kipindi cha Laodikia? Angalia Ufu. 3:14-17.
7. Ni ushauri gani wanapewa wale walio katika hali ya uvuguvugu? Ufunuo. 3:18, 19.
8. Je, ni ahadi gani imepeanwa kwa wale watakaofuata ushauri huu? Ufu. 3:20, 21.
9. Tukiongea kwa ujumla, tunatarajia hali kuwa njema au mbaya zaidi tunapokaribia mwisho? 2 Tim 3:13; 1 Tim 4:1, 2.



12. Watakao kuwa waaminifu kwa vitu vidogo watakuwa waaminifu kwa vitu vikubwa? Luka 16:10-13.

******************************

**Somo la Septemba 26, 2020 (Tishrei 8, 5781)**

## UFUFUO WA WAFU

**Somo kuu: Yohana 11:11-45.**
**Fungu la kukariri: Zab 17:15.**

1. Je, Yahshua alisemaje kuhusu ufufuo wa wafu? Yohana 5:25.
2. Je, wenye haki na wenye dhambi watafufuliwa katika wakati moja? Ufu. 20:5, 6
3. Je, Paulo alisemaje kuhusu ufufuo wa wafu? Matendo 24:15.
4. Ni lini ufufuo wa wenye haki utatendeka? 1 Thes. 4:16.
5. Ni kwa namna gani, na ni katika hali gani watafufuliwa? Zab. 17:15.
6. Je, watoto wadogo watafufuliwa? Yer. 31:15.
7. Je, Ayubu alisema nini kuhusu ufufuo? Ayubu 19:25-27.
8. Kunao ambao hawakuamini juu ya ufufuko wakati Masihi alikuwa duniani? Mathayo. 22:23; Luka 20:27.



4. Kitabu cha mwisho cha biblia kinaitwaje? Ufunuo 1:1.
5. Ni nini kimewekewa kwa wale watakaosoma unabii huu? Ufunuo 1:3.
6. Unabii wa agano la kale ulitolewaje? 2 Petro 1:21.
7. Nini kinachosemwa juu ya tafsiri ya unabii huu? 2 Petro 1:20.
8. Je, unabii huu unauhusiano wowote na unabii wa wokovu? 1 Petro 1:9-10.
9. Je, roho wa Masihi anauhusiano wowote na manabii? 1 Petro 1:11-13.
10. Ni kwa jinsi gani Masihi mwana wa Elohim alie hai alifunuliwa kwa Petro? 2 Petro 1:16, 17.
11. Ni kwa njia gani ya ajabu uwepo wake ulifunuliwa kwa Petro, Yakobo, and Yohana? 2 Petro 1:18; Mathayo 17:1-9
12. Ni kwa jinsi gani tutahuchukulia unabii huu wa ajabu kwa siku hizi na wakati huu wa sasa tunapoishi? 1 Kor 10:11; Warumi 15:4.
13. Petro, Yakobo, na Yohana, walipokea ufunuo wa kuja kwa Yahshua mara ya pili walipokuwa juu ya mlima mtakatifu. Lakini tuna nini hata leo juu ya kuja kwa Yahshua Masihi mara ya pili? 2 Petro 1:19.
14. Je mtu aliyeteuliwa kwa kweli, akaitwa kwa uzima wa milele, atafanikiwa au hatafanikiwa katika kazi ya Elohim kwa kipindi hiki? 2 Petro 1:8.

******************************

10. Je, ni onyo gani imepeanwa dhidi ya kupatikana na kuathiriwa na wimbi baya la uvuguvugu na roho ya kutojali? Luka 21:34-36; 2 Petr. 3:17.
11. Tukiwa wana wa kweli wa Elohim, ni nini lazima tupigane nayo? Efe 6:10-12; 5:11.

*******************************

**Somo la Agosti 8, 2020 (Av 18, 5780)**

## ALAMA YA MNYAMA

**Somo kuu: Ufunuo: 14:9-20.**
**Fungu la kukariri: Ufunuo 19:20.**

1. Kulingana na Danieli alama ya mnyama inaashiria nini katika unabii wa neno la Elohim? Danieli 7:17.
2. Je, baadhi ya sifa za mnyama zilizotajwa katika Ufunuo 13:11, ni gani?

**Maelezo**: Wafalme wasiomcha Elohim au watawala wanasimamia mnyama katika maandiko matakatifu. Naomba ukumbuke kila wakati biblia inapoongea kuhusu mnyama, jinsia ya kiume ndio inayotumika. Popote kanisa linapotajwa kwenye maandiko matakatifu jinsia ya kike hutumika.

3. Wakati mnyama anatawala nani atafanya kazi naye? Ufunuo 19:20.
4. Je, ni matukio gani ya muujiza ambayo shetani ataonesha kwa nguvu zake? Ufunuo 13: 13, 14



11. Je, kuna muda wa kipekee **ULIOTENGWA** kwa Bwana kuwapendelea Zayuni? Zab. 102:13
12. Je, ni nini kimesemwa kwa huu muda uliotengwa, na kuijenga upya Zayuni na kuja kwake Yahshua? Zaburi 102:16.
13. Wakati Wayahudi watarejeshwa tena, Je Bwana atawaweka wachungaji kwenye ardhi yao ili wawafundishe? Yer. 23:3, 4; 3:14, 15.

*******************************

**Somo la Agosti 29, 2020 (Elul 9, 5780)**

## YERUSALEMU, MJI ULIOPENDWA

**Somo kuu: 2 Mambo ya nyakati 5:1-14.**
**Fungu la kukariri: "Alipofika karibu, aliuona mji akaulilia." Luke 19:41.**

1. Jinsi gani eneo la hekalu la kwanza lilichaguliwa? 1 Nyakati. 21: 18-28
2. Ni katika kipindi gani hekalu lilijengwa katika eneo hilo? 2 Nyakati. 3:1, 2.

**MAELEZO:** Moriah, maana yake "Iliyotolewa na Yehova," na hii ililikuwa sehemu iliochaguliwa kwa maelekezo ya Elohim kupitia malaika kwa Daudi



**Somo la Julai 11, 2020 (Tamuz 19, 5780)**

## ISHARA ZA NYAKATI

**Somo kuu: Matayo 24:7-27.**
**Fungu la kukariri: 2 Timotheo 3:1.**

**MAELEZO:** Kuna unabii mwingi sana katika biblia unaozungumzia siku za mwisho. Tunaambiwa tukeshe na kuomba mambo haya yasitujie kama vile mwizi huja usiku. Bibilia inasema kwamba hakuna ajuaye siku au saa ya kuja kwake Mwokozi, hata hivyo tumepewa ishara nyingi zakutufanya tuwe tayari katika siku tunazoishi, siku za mwisho. Hebu tuone mambo waziwazi yaliyo rekodiwa kwenye biblia kwa ajili yetu, siku za zamani, za sasa na siku zijazo.

1. **KUSHUKA KWA ROHO MTAKATIFU** Matendo 2:17, soma pia Marko 16:17.
2. **KUACHA IMANI NA MAFUNDISHO YA UONGO** 1 Timotheo 4:1.
3. **KUTOAMINI NA WANAODHIHAKI**. 2 Petro 3:3.
4. **WADANGANYI WAKUU**. Mathayo 24:24.
5. **MAJANGA KATIKA DUNIA**. Luka 21:11 soma pia Mathayo 24:7.



3. Ilikuaje pale Paulo alipochaguliwa au kupokea huruma na msamaha baada ya kuwa amelitesa Kanisa? Matendo 9:1-17; 1 Tim. 1:13.
4. Je, Paulo aliteswa baada ya kuwa muumini wa kanisa la Elohim? 2 Kor. 11:24-27; Matendo 14:19.
5. Je, Paulo alisema nini kwa wale wote wanaoishi maisha ya haki katika Masihi Yahshua? 2 Tim. 3:12.
6. Kama muumini binafsi wa kanisa la Elohim, ni kutoka wapi tunaweza kutarajia mateso? Mathayo. 10:34-37.
7. Kama muungano katika mwili mmoja, ni kutoka wapi tunaweza kutarajia mateso? Matendo. 20:28-30; 2 Petro. 2:1-2; Mathayo. 24:11, 24.
8. Je, tunafaa kushangaa au kudhani ni jambo geni kama tutajaribiwa? 1 Petro 4:12.
9. Katika kuteseka, majaribu, na mateso, je tutakana au tutafurahia? Mstari 13, 14.
10. Je, kanisa litajaribiwa na mateso katika siku zinazokuja? Ufu. 12:17, pia sura ya 17:12-14.
11. Je, ni nini imesemwa kuhusu wale waliokolewa katika siku hizi za mwisho za mateso? Mstari 14 sehemu ya mwisho.

**MAELEZO.** Hatua tatu zimetajwa hapa kutuhitimisha kuwa "Bi arusi wa Masihi" - kuitwa, kuchaguliwa na kuwa waaminifu.

**Somo la Agosti 22, 2020 (Elul 2, 5780)**

# KUKUSANYWA KWA TAIFA LA WAYAHUDI

**Somo kuu: Kumbukumbu. 30:1-15.**
**Fungu la kukariri: Kumbukumbu. 30:19.**

1. Je, Elohim aliwaahidi Wayahudi kurudi kwenye nchi yao? Yer. 24:5-7.
2. Je, ni ahadi gani nyingine tunayo kuwa Wayahudi watakusanywa? Yer. 32:37-44.
3. Je, miji iliyoharibiwa itajengwa tena? Eze. 36:33, 36; 38:10-12
4. Yeremia alisema nini zaidi kuhusu Wayahudi? Yer. 30:18-21.
5. Je, vita vitaendelea hadi sasa? Yer. 30:23, 24.
6. Je, ardhi itapandwa na nyumba zitajengwa tena? Amosi 9:14, 15.
7. Kukusanywa kwao mara ya kwanza kulifuatia mwaka wa 457 B.C. Ezra 7. Je, walikuwa wakusanywe kwa mara ya pili? Isa. 11:11, 12.
8. Je, Musa alitabiri nini kuhusu Wayahudi? Kumbukumbu. 30:19, 20.
9. Je, ni nini kitatokea baada ya wayahudi kurejeshwa Yerusalemu? Yoeli 3:1, 2; Zekaria. 14:1-4.
10. Je, Elohim aliwaambia Wayahudi atawatendea nini? Zekaria. 8:12-15.



5. Je, Yahshua alisema nini juu ya nguvu za shetani zitakazokuwepo kabla ya kuja kwake mara ya pili? Mathayo 24: 2
6. Jinsi gani mtume Paulo alielezea yule mwovu, na alisema nini kuhusu nguvu za kishetani atakazomiliki? 2 Wathesalonike 2: 8-10.
7. Wakati wa utawala wa nguvu za yule mwovu, ni mamlaka gani atatumia kwa watakaoishi kwenye utawala wake? Kwa ambao watalazimishwa kumwabudu? Ufunuo 13: 12.

   **MAELEZO**: Tunaona kuwa huyu mnyama aliyeongozwa na Shetani atatumia nguvu za mnyama wa kwanza, yule kanisa liloanguka lilipanda.

8. Je, ni nguvu gani ya ajabu nabii wa uongo atamiliki ambaye hufanya kazi pamoja na mnyama? Ufunuo 13: 15.

   **MAELEZO:** Nebukadineza aliamuru sanamu itengenezwe katika wakati wa Danieli. Lakini sanamu ile ilikuwa haina uhai wala haiongei. Lakini sanamu ya Ufunuo 13:15 itakuwa na uwezo wa kufanya matangazo yake.

9. Je nguvu za shetani zilizaa uhai kabla ya siku za huyu mnyama? Kutoka 7: 11, 12; 8:7.
10. Ni kwa njia gani wote waliojiingiza kwenye nguvu za huu uovu watafahamika? Ufunuo 13:16.



5. Je, nabii Zekaria anasema nini kuhusu Israeli kuwa kiini cha ubishani miongoni mwa mataifa? Zekaria 12:2, 3.
6. Je, Wayahudi watakuwa katika Yerusalemu katika kipindi hiki? Nini imesemwa kuhusu nguvu yao katika kushinda? Mstari 6.
7. Kabla ya siku ya mwisho ya onyesho kuja, na mataifa kukusanyika dhidi ya Yerusalemu kwa hukumu, kazi ya kiroho itakuwa imekwisha juu ya Wayahudi? Mstari 7.
8. Jinsi gani huu ubishi dhidi ya Zayuni utaisha? Zekaria 14:1-3; Yoeli 3:16, 17.
9. Nini kitatokea kwa watu ambao watakuwa kinyume na Yerusalemu? Zekaria 14:12.
10. Ni adhabu gani mataifa watapata wale ambao hawatamkubali Yahshua Masihi kama Mfalme? Mstari 16, 17.

********************************

**Somo la Septemba 19, 2020 (Tishrei 1, 5781)**

# KUTESWA KWA KANISA

**Somo kuu: Matendo 9:1-18.**
**Fungu la kukariri: Matendo 22:4.**

1. Mtume Paulo alilitazamaje kanisa katika wakati fulani? Wagal. 1:13; Matendo. 8:1-3.
2. Kwa sababu ya Paulo kulitesa Kanisa la Elohim, alijisikiaje kuteuliwa kama mtume? 1 Wakor. 15:9.



6. **NYAKATI NGUMU DUNIANI**. 2 Timotheo 3:1.
7. **KUZALIWA UPYA KWA ISRAELI**. Mika 4:1 soma pia Yeremia 29:14.
8. **KUBADILIKA KWA MAUMBILE.** Luka 21:25.
9. **ROHO YA MPINGA MASIHI**. 2 Thesalonike 2:9 soma pia 1 Yohana 4:3 na 2 Yohana 1:7.
10. Tutajua muda wa kuja kwake? Matendo 1:7.
11. Nini kimeahidiwa kwa wale wanaopokea na kuyashika maneno ya kinabii na ahadi zilizo ndani yake? ufunuo 1:3.
12. Je! Ni ujumbe upi kwa dunia katika siku hizi za mwisho? Marko 1:15.

********************************

**Somo la Julai 18, 2020 (Tamuz 26, 5780)**

# KAMA ILIVYOKUWA SIKU ZA NUHU

**Somo Kuu: Mathayo 24:1-51.**
**Fungu la kukariri: Mathayo 24:37.**

1. Wakati mmoja Yahshua alikuwa katika mlima wa mizeituni, wanafunzi wake walimuuliza nini? Mathayo. 24:3.
2. Jinsi gani Yahshua alifananisha siku kabla ya kurudi kwake? Mathayo 24:37.

11. Je, ni hatima gani inayowangoja wale wanaoishi katika utawala wa mnyama na wale wanaokataa kumwabudu? Ufunuo 13:15, 17.
12. Jinsi gani huyu mnyama atatambulika? Ufunuo 13:18.
13. Je, nguvu hizi ovu zitakuwepo wakati Yahshua atarudi katika dunia? Ufunuo19:11, 14, 19.
14. Je, mwisho wa mnyama utakuwa upi? Ufunuo 19:20.

******************************

**Somo la Agosti 15, 2020 (Av 25, 5780)**

## ISRAELI NA MAJIRA YA MATAIFA

**Somo kuu: Luka 21:24-38.**
**Fungu la kukariri: Luka 21:36.**

1. Je, Yahshua alisema nini juu ya mateso ya Wayahudi na kipindi cha kutawanyika kwao? Luka 21:24.
2. Kama nyakati za mataifa zinaelekea mwisho, ni hali zipi zitaitawala dunia? Mistari 25, 26.

**MAELEZO**. — Majira ya mataifa hayakuanza katika siku fulani, au hata mwaka fulani, bali ni katika kipindi cha wakati. Kama vile Waisraeli walipoteza hamu na kuingia katika hali ya kutoamini, watu wa mataifa wakawa na hamu. Leo haya yanatendeka kinyume: watu wa mataifa kwa



haraka wanamgeuka Bwana. na Israeli wanakuwa na hamu.

3. Ni kwa kipindi gani Yerusalemu itakanyangwa na watu wa mataifa? Luka 21:24.
4. Ni kwa muda gani upofu utabakia kwa Waisraeli na Wayahudi? Warumi 11:25.
5. Je, Bwana atawapokea Waisraeli tena na kuwapandikiza kwenye mzeituni wa shamba? Warumi 11:23, 24.
6. Jinsi gani kupokelewa kwao kunahusishwa na ufufuko? Mstari 15.
7. Kulingana na nabii Ezekieli, wakati Israeli watarudi kwenye nchi yao, wao pia watapewa roho, na kubadilishwa kwa moyo? Ezekieli 36:24-26.
8. Je, ni hali zipi zitatawala nchi ya Israeli kuhusu kunyunyiziwa maji safi (neno) kwa Wayahudi? Mstari 25.
9. Wakati Bwana Yahshua atarudi juu ya mlima wa Mzeituni, Je atakuja kwa ajili ya wanaoishi katika dhambi au atakuja kwa wale waligeuka na kuacha uovu? Isaya 59:20.
10. Je, itakuwa baada ya kuja kwa Yahshua, Israeli watamtafuta Bwana hapa Yerusalemu? Au itakuwa "katika siku za mwisho"? Hosea 3:4, 5: 5:15.
11. Baada ya Bwana kuwakusanya Wayahudi kurudi kwenye nchi ya Israeli, atawatuma wachungaji wawafundishe njia za haki? Yeremia 3:14, 15.

******************************



3. Baadhi ya dhambi wakati wa siku za Nuhu zilikuwa gani? Mathayo. 24:38; Luke 17:26-27.
4. Ni uovu gani wa binadamu unaoelezewa katika kitabu cha mwanzo 6:2, 5, 11-13?
5. Katika maovu katika hizo siku, ni nani pekee yake, na nyumba yake walibaki kuwa waaminifu? Mwanzo. 7:1.
6. Mtume Paulo alizungumza nini kuhusu Nuhu? Waebrania. 11:7.
7. Ni kupitia kwa nani Elohim alionya watu katika wakati huo, wakati maasi yalikuwa makubwa? 2 Petro. 2:5.
8. Nini kilitokea baada ya Bwana kumwita Nuhu na watu wa nyumba yake katika safina? Mwanzo. 7:4, 11-12.
9. Ni kwa kiwango gani kulikuwa na ukamilifu katika kuangamiza viumbe viote? Mwanzo. 7:21-23.
10. Ni kwa nani Petro alizungumza kuwa uharibifu wa wakati wa Nuhu na Lutu, umetolewa kama mfano? 2 Petro 2:5, 6.
11. Dunia ovu iliangamizwa kwa maji wakati wa Nuhu. Maandiko yanasemaje, ni nini kitatokea kwa Dunia ovu wakati ujao? 2 Petro 3:6,7,10.
12. Baada ya dhambi na watenda dhambi kuwa wameharibiwa, na dunia kuwa imesafishwa kwa moto, nini kitakuwa kimekamilika? 2 Petro3:11-13; Isaya. 65:17.

******************************



**Somo la septemba 12, 2020 (Elul 23, 5780)**

## KUWEKA HATUA KWA ARMAGEDDON

**Somo kuu: Yoeli 3.**
**Fungu la kukariri Yoeli 3:9.**

1. Kabla ya mataifa kuletwa katika hukumu, katika Yerusalemu ni kabila lipi litakuwepo? Yoeli 3:1; Zekaria 12:2.

**MAELEZO**. — Bonde la Yehoshefati lipo kati ya Yerusalemu na mlima wa Mizeituni. Ni bonde refu na lina kina kirefu.

2. Ni kwa muda gani Yahshua alisema Wayahudi watakuwa katika mateka? Luka 21:24.
3. Je, ni hali gani alisema zitatawala dunia wakati wa mataifa utakuwa unafika mwisho? Luka 21:26, 27.
4. Je, ni nini nabii Isaya anatuambia kuhusu kuisha kwa utawala wa watu wa mataifa? Isaya 34:1-5 (aangalia katika ukurusa juu).

**MAELEZO.** — Idumea (au Edomu) ni nchi ya kiarabu, kwa sasa imeizunguka Israeli, ambayo inakusudia kuwaangamiza Waisraeli.